102/2 MK
KCSE
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA
MACHI 2022

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION

KISWAHILI

KARATASI YA 2

**Mwongozo wa Kusahihishia**
**(SIRI)**

Teacher.co.ke

**MWONGOZO HUU WA KUSAHIHISHIA NI MILKI YA BARAZA LA MITIHANI YA KITAIFA LA KENYA (KNEC) NA SHARTI KUREJESHWA KWA BARAZA HILI BAADA YA USAHIHISHAJI.**

**Mwongozo huu wa kusahihishia una kurasa 9 zilizopigwa chapa.**

©2021 The Kenya National Examinations Council

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Scanned with CamScanner

1. UTAHAMU

**(a) Mambo yanayoleta utangamano katika jamii hii;**

(i) Kuketi nje jioni na kunywa kahawa pamoja.

(ii) Kufanya vikao kuwa vya kikaida kuliwawezesha kukutana kila mara.

(iii) Kufanya mjadala pamoja kuhusu masuala yaliyowaathiri.

(iv) Kuwa na hali sawa/ changamoto sawa zilizowazunguka, kama vile haja ya kuboresha matibabu, miundomsingi na makazi.

(v) Kuwa na muono / Hali ya kujali maendeleo ya nchi yao iliwaleta pamoja. Msimulizi anasema wapo ili kuzungumzia nguzo kuu za maendeleo.

(vi) Kuyadhibiti maingiliano/ mazungumzo yao/ kuwa na utaratibu maalum wa kuendeshea mazungumzo yao/. Kuwa na kiongozi/mwendesha mjadala aliyewapa nafasi za kuzungumza katika nafasi maalum kuliwasaidia kukinga dhidi ya kutoelewana.

**Hoja 3 x 1 = 3**

**Tanbihi**

Hili ni swali la ufasiri. Mtahini atathmini majibu ya mtahiniwa.

**(b) Mambo yanayoonyesha kuwa kupata elimu tu hakuwezi kuleta maendeleo**

(i) Elimu ya nadharia – hivyo haisaidii.

(ii) Elimu isipotumiwa kuzalisha haina maana – elimu haina maana ikiwa kuipata kutatazamwa kama hatima ya mambo.

**Hoja 2 x 1 = 2**

**(c) Uhusiano kati ya nguzo mbalimbali za maendeleo**

(i) Afya na viwanda – watu wanaweza tu kufanya kazi vizuri wakiwa na afya.

(ii) Viwanda na miondomsingi – bidhaa huweza kufika na kutoka mahali mbalimbali na ahata kuzalishwa kwa kuwa na miondombinu /miondomsingi ifaayo.

(iii) Makao ya watu ni muhimu kwa wafanyakazi ambao huhitaji kupumzika vizuri ili kufanya kazi.

(iv) Elimu ni muhimu katika kupata maarifa ya kujenga viwanda na miondomsingi

(v) Elimu inahitaji nyanja nyingine kama vile viwanda ili kupata baadhi ya vifaa kama vile kalamu.



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke
Scanned with CamScanner

(vi) Binadamu mwenye elimu anahitaji kuwa na afya na kuishi mahali panapofaa ili kuweza kuzalisha mali ipasavyo.

**4 x 1 = 4**

**(d) Mambo matatu yaliyowachangamsha vijana**

(i) Mbwembwe za Sumaku wakati wa kusema

(ii) Hoja za Sumaku zizowatetea vijana

(iii) Hatua ya mzee kujiondokea bila kuaga

**3 x 1 = 3**

(e) Tashhisi/uhuishaji/uhaishaji – upepo kupewa sifa ya kibinadamu ya kupapasa

Chuku – haiwezekani katika hali ya kawaida kwa upepo kupapasa

**1 x 1 = 1**

(f) Tulinoleana bongo – tulielimishana/tulitoleana maarifa/ tulierevushana/tulifunzana

**1 x 1 = 1**

(g) hoja – rai, wazo, fikra, shauri

**1 x 1 = 1**

**Tanbihi**

Mwongozo wa kudumu pia uzingatiwe katika utuzaji.

Teacher.co.ke

## 2. UFUPISHO

(a)

(i) Binadamu aliumbwa kushirikiana na wenzake.

(ii) Asili ya familia ni uumbaji alioufanya Mungu ili wasaidiane.

(iii) Ushirikiano wa familia ni muhimu tangu enzi za mababu zetu ambapo watu waliungana kupambana na adui na wanyama hatari.

(iv) Baadhi ya koo zilikuwa na uhasama kwa kushindania mifugo.

(v) Kujihami kwa familia kuliwahakikishia watu utulivu.

(vi) Ushirikiano ni muhimu hata miongoni mwa wanyama ili kujifadhi.

**Hoja 5 x 1 = 5**

**Alama 1 ya mtiririko (Jumla: alama 6)**



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Scanned with CamScanner

(b)

(i) Ushirikiano leo hii upo katika taasisi mbalimbali.

(ii) Wanafunzi hufaidi ushirikiano mzuri wakiwepo shuleni .

(iii) Manufaa ya ushirikiano shuleni huja kwa mwanafunzi kulenga kimaksudi kuwa mtu bora.

(iv) Ushirikiano huja kwa mtu kufanya juhudi za kimakusudi.

(v) Taasisi zetu muhimu hutegemea ushirikiano uliojengwa katika misingi ya kifamilia ili kufanikiwa.

(vi) Katika taasisi watu huja pamoja kuunda kanuni za kuendeshea mambo.

(vii) Ulimwengu wa leo unahitaji watu wawezao kushirikiana.

(viii) Uzalishaji huwa mkubwa watu washirikianapo.

(ix) Mtu ajitengaye na wengine huhangaika kutekeleza majukumu yake.

(x) Ushirkiano humfanya mwanafunzi kuwa wa kutegemewa zaidi.

(xi) Ushirikiano huokoa muda.

(xii) Ushirikiano huboresha uzalishaji.

**Hoja 8 x 1 = 8**

**Alama 1 ya mtiririko (Jumla: alama 9)**

Teacher.co.ke

### 3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) (i) /l/ - kitambaza

/r/ - kimadende

(ii) /m/ - nazali/king'ong'o

/b/ - kipasuo

**2 x 1 = 2**

(b) (i) wingi/ nafsi ya tatu-wingi/ nyinyi

(ii) nafsi ya kwanza- umoja/mimi/mtendwa

**2 x ½ = 1**

(c) Mkanda, mlango, mkondo.

**1 x 1 = 1**



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Scanned with CamScanner

Teacher.co.ke

**1 / 0**

(d) Kiunganishi kitegemezi huunganisha vishazi vyenye hadhi tofauti: kishazi huru na kishazi tegemezi.

Sentensi ibainishe viunganishi kama vile; ingawa, licha ya, iwapo, kama, ikiwa, pamoja na, minghairi ya . Baadhi ya mifano:

(i) **Kama** angefika mapema angenikuta.

(ii) **Iwapo** unataka ufanisi tia bidi.

(iii) **Ingawa** ana uwezo tunamsaidia.

(iv) **Licha ya** cheo chake, hakuisaidia jamii yake.

(v) Utaliinua gogo hilo **ikiwa** utakubali kusaidiana na wenzako.

(vi) Alihudhuria hafla hiyo **mingairi ya** kuonywa na wenzake.

**1 x 2 = 2**

**2/0**

(e) (i) Kiwakilishi;

i) Huyu anataka vile.

ii) Vile ni vyake.

iii) Mpe vile.

**1 x 1 = 1**

(ii) Kielezi :

i) Mbona unamtazama vile?

ii) Umesikia vile alivyosema?

**1 x 1 = 1**

(f) (i) Nomino - werevu – alama 1

(ii) Kivumishi - mwerevu- alama 1

(g) (i) teo – U – ZI/ ZI – alama 1

(ii) chanda - KI-VI/VI- alama 1

( 2x1)



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Scanned with CamScanner

Kirai Mambo yanayofanya kazi pamoja
Neno kuu ndilo linatupa ~~mao~~ aina ya kirai

(h) wale wengine – kirai nomino
watasafiri ughaibuni – kirai tenzi / watasafiri ughaibuni kwa ndege (kirai tenzi) 3
kwa ndege. kirai kihusishi /kirai husishi
3x 1 = 3

(i) Nguo aliyouza dukani mwake ilimvutia mtalii.
1 x 1 = 1/ 0 Akikosea sehemu yoyote (0)

(j) Makuli wamekuarifu kwamba mizigo hiyo ilikuwa yetu?
1 x 1 = 1/ 0

(k) Lo! Kadio, Hamadi ndiye mwandishi wa Kisiwa chenye Tunu?! Moja ikikosa hapati alama.

Au

Lo! Kadio Hamadi ndiye mwandishi wa Kisiwa chenye Tunu?!
~~1 x 2 = 2 (2/0)~~ ½ x 4 = 2

(l) "Juma! Juma! Umefaulu vipi kuuzima moto huu?" Mama akauliza

au

"Juma," mama akaita, "umefaulu vipi kuuzima moto huu/huo?" alifaulu vipi kuzima moto huo.
1 x 2 = 2 ( 2/ 0) (Lazima atumie alama za ufunguzi)

(m) (i) Mbao zililainishiwa kiwandani na seremala. (pale/seremala) (kiwandani)

Au

(ii) Mbao zililainishwa na seremala akiwa kiwandani.
1 x 2 ( 2/ 0)
(iii) Mbao zililainishwa na seremala aliyekuwa kiwandani.
(iv) Mbao zililainishwa na seremala alipokuwa kiwandani.

(n) Punde tu alipojibu swali hilo Koru alitoka darasani.
alipoulizwa ghafla alitandoka.
1 x 1 = ~~1/0~~ 2 x ½ = 1

(o) (i) Jani ambalo hupukutika hupeperushwa na upepo.
(ii) Jani lipukutikalo hupeperushwa na upepo.
(iii) Jani linalopukutika linapeperushwa na upepo.
(iv) Jani linalopukutika hupeperushwa na upepo.
Jani lipukutikalo huwa linapeperushwa.
1 x 1 = 1

(p) S→KN (N+V) +KT (T+N+V+E)

au

S→KN (N+V)+KT(T+KN(N+V)+E

au



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke
Scanned with CamScanner

Kwa matawi ale jedwali (S) lazima izingatiwe

S→KN+KT

✓ KN→N+V

N→ Wakulima

V→hawa

✓ KT→T+KN+E

T→wanapanda

KN→N+V

N→zao

V→hili

E→daima

$4 \times \frac{1}{2} = 2$

(q) Babu alinyweshwa uji na Andai kwa kikombe.

Babu alinyweshwa uji kwa kikombe na Andai

1 x 1 = 1 (1/0)

(r) Sentensi inaweza kubainisha mbili kati ya maana hizi:

(i) mpango wa mafundisho wa elimu maalum

(ii) kipindi cha mafundisho au mazoezi

(iii)mtu mwenye jina moja na mwingine/ mwenye jina sawa na lako

(iv)mwalimu afundishaye mambo ya kunga unyagoni au kumbini/kungwi

(v) rafiki

1 x 2 = 2 → 2/0

Sentensi lazima iwe maana bayana basi isipotoa maana mbili, wazi apate moja (1)

(s) (i) **Sehemu ya kitu:**

Wanafunzi wawili kwa kumi huchelewa kila siku.

**Au**

Alipata themanini kwa mia katika jaribio hilo.

ii) **Namna ya kutenda jambo**

Tindi alimtazama kwa huruma.

**Au**

Ndua anakata kuni kwa upanga.

**2 x 1 = 2**

(t) Ukuta uliojengwa kwa mawe ulidumu.
**tegemezi** **huru**

Vigezo vya vishazi tegemezi
Sentensi iwe changamano
iwe na kitenzi kishirikishi
Ki ya masharti
Matumizi ya po ya masharti
kwa haraka



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke
Scanned with CamScanner

Teacher.co.ke

Au

Ukuta ukijengwa kwa mawe — utadumu.
tegemezi — huru

Au

Maria alitia bidii masomoni — akafaulu.
huru — tegemezi

Ingawa alikuwa na mahitaji maalumu — alijitahidi maishani.
tegemezi — huru

~~1 x 2 = 2~~

u) Maana

i) Fundi alikata utepe akampa Makaa- kwa faida ya Makaa.

ii) Fundi alikata utepe kwa niaba ya Makaa/ badala ya Makaa kuukata utepe.

iii) Fundi alimkata Makaa kwa sababu ya utepe.

iv) Fundi alikata utepe wa Makaa ili kumhasiri ~~Maria/~~ ili kumuumiza Makaa.

v) Fundi alimakata Makaa kwa kutumia utepe.

2x1 = 2

v) Kadiri zimwi lilivyozidi kukimbia ndivyo shujaa/Shujaa alivyoongeza mwendo kulifikia.

w)

i) **Mifano ya sentensi agizi**

i) Njoo hapa!

ii) Meza tembe mbili mara tatu kwa siku.

iii) Tembea hatua tatu kuelekea kushoto kisha upinde kulia.

iv) Unaweza kunipitishia bilauri hiyo?

1x1 = 1

ii) **Mifano ya sentensi hisishi ( inayoibua hisia)**

i) Maskini, hakuliona gogo hilo, sasa limemuumiza.

ii) Ni moyo wa nani usiohuzunika kwa tendo kama hilo?



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Scanned with CamScanner

iii) Jamani/Maskini! Anaonekana kuzidiwa na msiba.

iv) Sasa nitafanya nini mimi mnyonge nisiyemjua yeyote?

## 4 ISIMUJAMII

(a) (i) Mahojiano kati ya mwajiri na mwajiriwa/ Sajili ya Mahojiano.
**1 x 1**

**Tanbihi**

(Atakayeandika ni sajili ya mazungumzo , **asituzwe.)**

(a) (ii)

(i) Kuna istilahi/msamiati maalum wa mahojiano. Kwa mfano, jopo, kujitambulisha kwa jopo, nafasi.

(ii) Lugha dadisi. Ni jambo gani linalokufanya uamini kwamba nafasi hii inakuafiki wewe?

(iii) Kuzungumza moja kwa moja na mhojiwa. Kwa mfano, Bwana Nuru.

(iv) Lugha ya heshima. Karibu! Karibu keti.

(v) Ni lugha, rasmi. Kwa mfano, **'Bwana** Nuru'.

(vi) Ni lugha inayozingatia kanuni za kisarufi. Kwa mfano, nafasi hii inakuafiki ..."

(vii) Kuna matumizi ya sentensi ndefu ndefu hasa kwa upande wa maswali ya mhoji K.m. Bwana Nuru ni jambo lipi ambalo ....

(viii) Mahojiano kuzingatia utaratibu fulani. Kwa mfano, kukaribishwa, kujitambulisha na kuulizwa maswali.

**Hoja 4 x 1 = 4**

4(b) Hii ni sajili ya matangazo ya mchezo wa kuogelea. Sifa za matangazo ya aina hii zijitokeze. Baadhi ya hoja ni:

(i) Kuzungumza moja kwa moja na hadhira.

(ii) Kutumia msamiati maalum wa uogeleaji. K.m. piga mbizi, *free style*.

(iii) Kuchanganya ndimi. Kwa mfano, mtindo wa '*free style*', *backstroke*.

(iv) Lugha yenye kupiga chuku. Kwa mfano, 'Anampiku samaki katika uogeleaji'.

(v) Lugha ya kusisimua/kuvutia. K.m. Haya , haya mtazamaji. Ndiye huyo duma kwenye kidimbwi, jitazamie mwenyewe, ukimkosa utakonda....

(vi) Ni mazungumzo ya kasi kutokana na kasi ya uogeleaji.

(vii) Sentensi fupifupi/lugha ya mkato, k.m. Huyoo! Amempita Pendo.



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke
Scanned with CamScanner

(viii) Kutaja waogeleaji kwa majina yao/majina ya lakabu au hata majina ya timu. K.m. Papa wa baharini, Pendo, gwiji.

(ix) Wakati mwingine kuna kuvunja kwa sheria za kisarufi au matumizi ya kikaida ya lugha. lagova / isiyo sanifu

(x) Kutumia lugha ya kitamathali inayomjengea picha msikilizaji. Kutumia tashbihi istiara, methali. K.m. anapiga mbizi kama samaki ziwani. Huyu ni papa hasa.

(xi) Lugha yenye porojo, k.m mfuatano wa maneno ambayo huenda yasiwe na maana katika matumizi ya kawaida.

**Hoja 5 x 1 = 5**

XII Maswali ya balagha hutumiwa
XIII Uradidi / Takriri kusisitiza
XIV Lugha ya vihisishi
XV Lugha ya kiimbo cha juu

Sifa na mfano alama ½ na ½
Tano za mwanzo.
Unasema na kumwondoa alama za sanifu 4 na hija 4
Katika sehemu ya (a) na (b)

(a) Makosa yatolewe kwa mifano.
(b) Makosa ya mfano yasiondolewe (mfano yake) Tutapuuza mfano.

Makosa ya Kisarufi



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke
Scanned with CamScanner

## Makosa ya Sarufi

i) Miundo mibaya ya sentensi [?] / Minyambuliko mibaya
ii) Mwandiko mibaya ya vitakifishi
iii) Matumizi mabaya ya vitakifishi.
iv) Kutoakifisha
v) Matumizi ya herufi ndogo
vi) Matumizi ~~[illegible]~~ mabaya ya herufi kubwa
vii) Kuruka neno katika sentensi
viii) Kurudia neno.
ix) Kutumia aina ya neno lisilofaa. (mfano alisafiri na miguu)
x) Upatanisho usiofaa.
XI Changanya nyakati.
XII Kuchanganya nafsi (Yeye ninakula).
XIII Kutoambisha

## Makosa ya hijai/tahajia

i) Kudondosha herufi au kuacha herufi katika neno (hakuna akuna)
ii) Kuongeza herufi (jana) (njana) ~~au mwandiko au mambo yasiyofaa~~.
iii) Kubadilisha herufi liwe wazi
iv) Kutenganisha maneno (m
v) Kuunganisha
VI Kutumia vifupisho
VII Matumizi mabaya ya ritifaa/kutotumia.
viii) Kuandika neno vibaya lililochapishwa katika mtihani
IX ~~[illegible]~~ Mambo mabaya ya herufi.

Teacher.co.ke

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Scanned with CamScanner

# Ufupisho

(a) i Binadamu hakuubwa kuishi katika upweke.
ii Mungu alimuumba mwanamke na mwanamume washirikiane.
(iii) Hatua hii ikawa kiini cha familia.
(iv) Mshikamano wa familia hujenga uhusiano mwema/uhusiano au mshikamano wa familia ni muhimu
(v) Mababu walitaji umoja ili kujikinga dhidi ya wanyama
VI Enzi za mababu zilishuhudia uhasama wa kikoo.
VII Ushirikiano wa kanbu ulitajika ili kujihami dhidi uvamizi
VIII Utulivu wa jamii ulikuwa msingi wa maendeleo
(IX) Utulivu uliwapa watoto mazingira salama wa kukua na kukua.
(X) Ushirikiana pia upo miongoni mwa wanyama
(XI) Ushirikiano huu huwasaidia kujikinga katika hatari
(XII) Aidha huwasaidia kupata riziki

B) i) Watu hawashirikiani katika familia tu bali katika pia shule.
(ii) Shuleni watu wanapokezana maarifa mbalimbali ambayo ni muhimu katika maisha yajayo.
iii) Ushirikiano mzuri humfaidi mwanafunzi/humpa faida teknolojia anachokitumia kwa
(IV) Mwanafunzi hukuza kipawa chake manufaa yake na jamii.
V Maarifa hupatikana kwa mwanafunzi kujenga uthabiti wa fikra ya kulenga kwa kwa wenzake au mazoea ya daima
(VI) Taasisi za kuendesha maisha yetu yanajengwa katika misingi ya familia
Vii) Watu hufanya sheria zinazoelekeza utendaji kazi wao, huduma zingekwama.
(viii) Bila mpangilio huduma zingekwama.
ix Ulimwengu wa sasa unahitaji ushirikiano
x Ushirikiano hufanya shughuli nyepesi,
xi Binadamu ana wajibu maalum kutokelezo kwa kushirikiana na wenzetu
XII Mtu akijitenga mzigo wa safari utakuwa mzito kwake



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke
Scanned with CamScanner